

TANGAZO



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



Katibu Mtendaji, Baraza la Mitihani la Tanzania anapenda kuwajulisha watu wote wanaotarajia kufanya Mtihani wa **Kidato cha Sita (ACSEE)** mwezi **Mei 2023** kama Watahiniwa wa Kujitegemea kwamba;

1. Kipindi cha kawaida cha usajili wa Watahiniwa wa Kujitegemea kitakuwa kuanzia tarehe **01 Julai** hadi **30 Septemba, 2022** kwa ada ya Shilingi **50,000/=**. Aidha, watakojisajili kwa **kuchelewa** yaani kuanzia tarehe **01 Oktoba** hadi **31 Oktoba, 2022** watalipa Shilingi **65,000/=** ikiwa ni ada ya kawaida pamoja na faini.
2. Usajili utafanyika kwa njia ya mtandao (**online**). Aidha, kabla ya kujisajili, waombaji wanapaswa kwenda kwenye Vituo vya Mitihani kuchukua **Namba Rejea (Reference Number)** zinazotolewa **bure na** kufanya malipo ya ada kupitia Posta au Benki kwa kutumia 'Control Number'.
3. Ufafanuzi kuhusu utaratibu na hatua za kufuata katika kutengeneza '**Control Number**' na kujisajili, umetolewa katika tovuti ya Baraza la Mitihani la Tanzania: www.necta.go.tz. Aidha, kwa watahiniwa ambao hawataweza kutumia mfumo huo wafike ofisi za Posta au wapige simu yenye namba **0738 785 945** kwa msaada zaidi.
4. Waombaji wote **wanasisitizwa** kuhakikisha wanajisajili mapema kwani mfumo wa usajili utafungwa baada ya kipindi cha usajili kukamilika.

Imetolewa na;

KATIBU MTENDAJI



Jiandae kuhesabiwa siku ya jumanne tarehe 23 Agosti, 2022

